

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MADINI

Telegramu "MADINI"

Simu: +255 26230051

Nukshi: +255 26 2322282

Barua Pepe: ps@madini.go.tz



Barabara ya Kikuyu,

S. L. P.422,

40474 DODOMA

TAARIFA KWA UMMA

TAARIFA YA MATOKEO YA MNADA WA TATU WA MAUZO YA ALMASI ZA MGODI WA WILLIAMSON DIAMONDS LIMITED

Wizara ya Madini inapenda kuutarifu umma kuwa, tarehe 2 hadi 9 Februari, 2018, Mnada wa Tatu (3) wa mauzo ya almasi kutoka Mgodi wa Mwadui unaomilikiwa na Kampuni ya Williamson Diamonds Limited ulifanyika mjini Antwerp, nchini Ubelgiji.

Katika mnada huo, jumla ya **Karati 54,094.47** ziliuzwa kwa thamani ya **Dola za Marekani 13,607,858.72** sawa na shilingi **30.6 Bilioni** ambapo jumla ya kampuni **145** zilishiriki katika mnada na kuwasilisha zabuni zao za ununuzi na zabuni **1,019** ziliwasilishwa katika mnada huo.

Kufuatia mauzo ya almasi hizo, Serikali imepata Mrabaha wa (Final Royalty) **Dola la Marekani 816,471.52** pamoja na Ada ya ukaguzi (*Clearance and Inspection*) kiasi cha **Dola za Marekani 136,078.59** sawa na shilingi za Kitanzania **2,090,164,095**.

Aidha, Mrabaha wa awali (Provisional Royalty) uliolipwa kutohama na uthaminishaji wa awali kabla ya mauzo ni **Dola za Marekani 674,941.78**, ada ya **Clearance** na **Inspection Dola za Marekani 112,490.30** pamoja na **Dola za Marekani 100** kwa ajili ya kibali cha kusafirishia almasi ambapo jumla yake ni **Dola za Marekani 787,532.08** sawa na **shilingi 1,771,947,000**.

Lengo letu ni kuanza mnada wa almasi hapa hapa nchini na tumeanza kulifanyia kazi.

Katika hatua nyingine, Wizara inapenda kuwafahamisha wananchi kuwa, ujenzi wa Ukuta kwenye mgodi wa Mirerani wenye urefu wa kilomita 24.5 kuwa upo katika hatua za mwisho kukamilika. Aidha, kuanzia siku ya **Jumatatu tarehe 19**

Februari, 2018, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kwa kushirikiana na Wataalam wa Wizara ya Madini wataanza zoezi la utoaji wa vitambulisho vya Uraia kwa wananchi wa eneo husika.

Zoezi hilo limelenga kuhakikisha kuwa wananchi watakaoingia katika eneo la usajili na utaoaji wa vitambulisho wawe wanatambulika kwa kuwa na vitambulisho ya uraia kwa kuwa lango la kuingilia katika eneo la migodi ya Tanzanite litakuwa moja tu. Hivyo, yejote asiyekuwa na kitambulisho hicho hataruhusiwa kuingia eneo la mgodi.

Aidha, Wizara inapenda kuwafahamisha wananchi na wadau katika sekta ya madini kuwa, kufuatia marekebisho ya Sheria ya Madini yaliyofanyika kuitia **The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, 2017** na kufuatia Kusainiwa kwa Kanuni za Madini za Mwaka 2018 na Waziri wa Madini, sasa vibali vya Usafirishaji wa Madini nje ya nchi (Export Permits), vitaombwa kwa Tume ya Madini na kusainiwa na Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Madini.

Aidha, vibali hivi vitaombwa kuanzia ngazi ya Mkoa. Hivyo, wadau wa sekta ya madini mnaombwa kuzingatia utaratibu huu katika kuomba vibali vya usafirishaji madini nje ya nchi.

Imetolewa na:

Doto Mashaka Biteko (MB)
Naibu Waziri wa Madini
16 Februari, 2018